JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI
S.L.P. 38 KYAKA - KAGERA

Kumb.Na.KGR/MSY/C.4/7/VOL.II/115 17 Aprili,2023

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi anawatangazia watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kuomba nafasi za kazi mbalimbali zilizotajwa hapa chini baada ya kupokea kibali cha ajira mpya kwa mwaka **2022/2023** chenye **Kumb. FA.97/228/01'TEMP'/06** cha tarehe **06 Aprili, 2023** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

## 1.0. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA III (NAFASI 23)

### 1.1. SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Elimu ya kidato cha IV, au VI aliyehitimu mafunzo ya Astashahada / cheti NTA LEVEL 5 katika moja ya fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo- Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali,

### 1.2. MAJUKUMU YA KAZI

i. Mtendaji na mshauri wa Halmashauri ya Kijiji na Kamati zake katika mipango ya maendeleo ya kijamii na utekelezaji wa mpango ya maendeleo.
ii. Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa mlizi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
iii. Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji na atakayesimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya Kijiji.
iv. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
v. Katibu wa Kamati ya Halmashauri ya Kijiji.
vi. Kutafsiri Sera, taratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogondogo katika Kijiji.
vii. Kusimamia na kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.

viii. Kuongoza vikao vya maendeleo ya kijiji vitakavyohusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake.
ix. Kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa na majanga mbalimbali.
x. Kusimamia matumizi bora ya nguvu kazi.
xi. Kuratibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika kijiji chake na kuziwasilisha kwenye Kata na kwa Mkurugenzi Mtendaji.
xii. Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na mwajiri.

## 1.3 NGAZI YA MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara wa TGS B sawa na Tsh. 450,000/= kwa mwezi.

## 2.0. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 6)

## 2.1. SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe na Elimu ya kidato cha Nne (Form IV)
ii. Awe na Leseni Daraja la E au C1 ya Uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali.
iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari 'Basic Driving Course" yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
iv. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

## 3.0. MAJUKUMU YA KAZI:-

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
vi. Kufanya usafi wa gari.
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

## 3.1. NGAZI YA MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara wa TGS B sawa na Tsh. 450,000/= kwa mwezi

**4.0. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE WA KAZI**

i. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45.

ii. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana muda wote pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

iii. Mwombaji aambatishe cheti cha kuzaliwa.

iv. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono.

v. Maombi yote yaambatane na cheti cha taaluma, maelezo Binafsi, na nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingaia sifa za kazi husika.

- Vyeti.
- Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
- Vyeti vya kitaaluma (Professional Certificates from respective board)
- Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni.

vi. Testimonials "provisional results" results slips ", kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa **HAVITAKUBALIWA.**

vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).

viii. Waombaji wa Nafasi za Ajira waliostaafishwa/ kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu kiongozi.

ix. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

x. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelezo yaliyo katika Waraka Na. **CAC.45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba, 2010.**

xi. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **02 Mei, 2023** saa **9:30** alasiri. Siku ya Jumanne.

xii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili hayatafikiriwa.

xiii. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo:-

xiv. Atatakiwa kuambatisha nakala ya kitambulisho cha uraia (NIDA) au namba ya NIDA kama hana kitambulisho.

Mkurugenzi mtendaji wa Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi,
S.L.P 38,
KYAKA- MISSENYI.

LIMETOLEWA NA:

Waziri K. Kombo
MKURUGENIZ MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI

Nakala : Mbao za Matangazo
: Tovuti ya Halmashauri www.missenyidc.go.tz
: Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira www.ajira.go.tz